Jarida la Wamama wa Maombi Kimataifa

Huduma ya Wamama ya Kanisa la Umoja Pentekoste

Novemba 2014

Wamama wa maombi kimataifa

Sisi ni nani… Wamama wa Maombi wa Kimataifa imeundwa na wanawake duniani kote tangu mwaka 1999. Wanawake hawa hukutana Jumatatu ya kwanza ya kila mwezi kuungana katika maombi kwaajili ya watoto wao na watoto wa kanisa la mtaa na jamii.

Dhamira yetu ... Nia yetu ni kuhifadhi kiroho kizazi hiki na zaidi, pia kurejesha kiroho vizazi vilivyopita

Haja yetu ... Wanawake watakaojiunga pamoja Jumatatu ya kwanza ya kila mwezi kuombea watoto wao.

Vipaumbele vitatu vya Maombi ...
1. Wokovu wa watoto wetu (Isaya 49:25; Zaburi 144:12, Isaya 43:5-6).
2. Kwamba wachukue umiliki wa imani katika umri wa kuwajibika (I Yohana 2:25-28; Yakobo 1:25).
3. Kwamba waingie katika huduma ya mavuno ya Bwana (Mathayo 9:38).

Moyo wa Shukrani

Glenda Alphin

"Nikiimba wimbo wa shukrani, na kusimulia matendo yako yote ya ajabu." Zaburi 26:7

Bado nakumbuka mara ya kwanza mmoja wa watoto wetu alipo kutana na nguvu ya uponyaji wa maombi. Sikuwa najisikia vizuri, na maumivu tumboni mwangu yalionekana kama yakiongezeka kila dakika. Binti yetu mwenye umri wa miaka sita, Candace, alipita kando ya chumba nilichokuwa nimeketi, na kwa hali mbaya, nikamwita na kumuuliza kama anaweza kuomba kwa ajili yangu. Alipoweka mkono wake mdogo juu ya kichwa changu, bado nakumbuka kuona uamuzi usoni mwake akimwomba Yesu aondoe maumivu yangu. Mguso wake ulikuwa papohapo! Nilishangazwa, lakini Candace hakushangaa. Alisali kwa matarajio, akiamini kwamba Yesu atafanya hasa alicho ombwa.

Moyo wangu hufurika na shukrani nikiangalia mchakato wa binti zetu wa ukuaji na mabadiliko. Kamwe sikufikiria kwamba hatimaye nitakuza watoto wa kimishenari; Hata hivyo, ningetambua kwamba Mungu alikuwa anapanga kitu fulani pale Yeye alipoweka wito wakimishenari kwa Candace akiwa na umri wa miaka mitano. Nikitafakari juu ya njia zake, siwezi kuzielewa . "Mtu ni nini, ee Mungu, hata umfikirie, binadamu ni nini hata umjali?" (Zaburi 8: 4). Ninapo kaa na kutafakari, karibu nashindwa na hisia.

Katika kipindi cha miaka kumi na tano iliyopita, naweza kuona ni jinsi gani maombi yamepeleka watoto wangu katika njia ya huduma. Nilimuona Miranda, mwenye umri wa miaka kumi na tatu, akiomba kwa ari kwa ajili ya

rafiki yake mpemdwa kupokea ufunuo wa wokovu. Kisha, nilimwona akilia kwa furaha pale rafiki huyo aliponena kwa lugha, na kuchukua jina la Yesu katika ubatizo. Nilimuona Candace akifundisha masomo yake ya kwanza ya Biblia akiwa na miaka nane, na kisha kuomba mara kwa mara kwa ajili ya rafiki yake mdogo kupokea Roho Mtakatifu mpaka yeye, pia, kupata jibu la sala zake.

Nimeona wasichana wetu wakiweka mikono yao juu ya watu, wakiamini kwa imani kwa ajili ya uponyaji, na kisha kulia kwa shukrani Mungu akijibu kila sala. "Yeyote anayempokea mtoto mmoja kama huyu kwa jina langu, ananipokea mimi" (Mathayo 18: 5). Naam, nami nashukuru.

Ukuaji wa kiroho wa namna hii hautokei siku kucha. Huja kutokana na miaka ya mifano mema kutoka kwa wengine. Ni matokeo ya mafundisho ya Neno thabiti (Kumbukumbu 6: 4-9). Ni ufahamu kwamba imani kweli huweza kuhamisha milima (Marko 11:23). Na hatimaye, ukuaji huanza pale watoto wetu wakitambua kwamba Mwenyezi Mungu anataka uhusiano binafsi nao (Mithali 8:17).

Nami namtukuza Mungu kwa yale aliyotenda na kwa yale atakayo tenda, kwa kuwa jambo hili moja najua: uaminifu wake ni mkuu! Hivyo, "Pitieni milango ya hekalu lake kwa shukrani, ingieni katika nyua zake kwa sifa. Mshukuruni na kulisifu jina lake. Mwenyezi-Mungu ni mwema; fadhili zake zadumu milele, na uaminifu wake katika vizazi vyote." (Zaburi 100: 3-5).

Kumbuka: Glenda hufanya kazi pamoja na mume wake, Mark, kama mmishenari nchini Finland. Yeye ni mwombezi na mwandishi. Miranda humwita "Momma," na kwa Candace, yeye ni "Mama."

Hivyo ndivyo Mama hufanya

Linda Elms

Mwaka 2010 kilitokea kitu sitasahau haraka. Mtoto wetu, Andrew alikuwa anajitayarisha kupanda farasi. Alipoketi juu ya farasi atakayempanda, nilifikiria jinsi gani alivyopendeza katika tandiko. Kisha, ghafla, farasi aliamua kupata hasira, nilichoona baada ya hapo ni Andrew akiwa ardhini na farasi akikanyaga kote karibu naye.

Moyo wangu ulisimama, lakini nikachukua hatua! Nilisema kwa sauti "Yesu," na kabla sijatambua, nilikimbia kuelekea kwa farasi. Najua farasi wana nguvu na wanaweza kukudhuru, lakini jambo hilo halikuwa la muhimu wakati huo. Cha muhimu ni kwamba mwanangu hakuwa anakanyagwa na farasi.

Nilipoona Andrew yu salama, nikapata utulivu. Kisha nikasikia mtoto wetu, Jonathan, akisema, "Mama, kitu cha mwisho unapaswa kufanya wakati kitu kama hiki kinapotokea ni kukimbia kuelekea kwa farasi." Nilijua alikuwa tu anajaribu kunilinda , lakini pia nilijua hakuwa na uelewa wa moyo wa mama. Kwa haraka nilimwambia kwamba nilishindwa kujizuia kuelekea kwa farasi.

Baadaye, Jonathan aliniambia tena. Kwa msisitizo nikasema, "Jonathan, hauelewi. Mama atafanya lolote linalobidi kufanya ili kulinda watoto wake." Mara nyingine tena, nikasema, "Nilishindwa kujizuia . Kulikuwa na msukumo ndani yangu uliyo nifanya kukimbia kuelekea kwa farasi ili kumlinda Andrew."

Nimekuwa relived kwamba wakati mara nyingi. Hata hivyo, lengo langu si hadithi ya "Farasi na Mpanda farasi". Bali ni ukweli kwamba Shetani anafanya kazi kwa muda wa ziada ili kuharibu maisha ya kiroho ya watoto wetu. Roho ya udanganyifu inataka kuiba ukweli nje ya nyoyo zao. Hata hivyo, kuna nguvu moja Shetani hataki kupambana nayo-sala za mama.

Akina mama, tunaweza kuwalinda watoto wetu dhidi ya mashambulizi ya Shetani tukiliita jina la Yesu. Endeleeni kuomba! Pambana kwa ajili ya watoto wako ukiwa magotini. Una uwezo wa kuangamiza kila pepo

kuzimu na uvamizi ambao umekuja dhidi ya mtoto wako. Ita jina la Yesu juu yao. Itia damu yake ya thamani. Fanya chochote unachopaswa kufanya kuwaweka salama kiroho. Maombi ni ufunguo wa ushindi katika nyumba yako na familia. Damu ya Yesu inakufunika wewe na huweka watoto wako salama. Kuna nguvu katika jina la Yesu.

Wakati wa msimu huu wa Shukrani nina shukuru kwa ajili ya jina la Yesu. Nina kushukuru katika nyakati za shida, ninacho hitaji kufanya tu ni kuita jina lake naye uwepo.

Kumbuka: Linda Elms ameolewa na Mchungaji Wendell Elms. Wana watoto wawili wa kiume, Jonathan na Andrew, ambao ni wachungaji wote wawili. Linda ni bibi kwa wajukuu sita wazuri. Kumtumikia Bwana kumekuwa mapigo ya moyo wake maishani. Linda amekuwa mzungumzaji mgeni katika maeneo mbalimbali nchini katika ushirika wetu. Ni mwanamuziki aliyefanikiwa na hupenda kuandika mara kwa mara kwenye blog yake.

Endelea tu Kuomba

Tiffini Countaway

Kama mtoto, kuna nyakati nalikuwa nahangaika au kupata kiu baada ya kuwekwa kitandani usiku. Kwenye pindi hizo, nilikuwa napita kwenye korido na kutembea mpaka sebuleni kumtafuta mama yangu kimya kimya nikipiga magoti kwenye kiti. Sikumbuki mara ya kwanza kumuona akipiga magoti kwenye kiti, lakini inaonekana kuwa kumkuta katika namna ile ilikuwa ni sehemu ya utoto wangu. Baada ya kumuambia mahitaji yangu, huinuka, hunidumia, na kunirudisha kitandani akinibusu. Yote yalikuwa mema tena.

Kwa miaka mingi sikuelewa nini alichokuwa anafanya akiwa amepiga magoti, lakini nilijua pa kumpata kama ikitokea kuwa mojawapo ya usiku wa kuhangaika. Kwa mbali nakumbuka nilipokuwa karibu na umri wa miaka nane hatimaye kumuuliza usiku mmoja kile alichokuwa anafanya, naye kimya kimya akajibu, "Nasali"

Nakubali kwa miaka mingi nilikuwa na changanywa na mama yangu akisali wakati wa usiku sebuleni kwetu . Baada ya siku ndefu ya kunihudumia mimi, baba yangu, nyumba, na mambo mengine mengi, kwa nini hakuenda kulala kama sisi wengine? Ni nini ambacho kilikuwa cha muhimu sana kumpasa akae usiku wote na kuomba? Hakika Mungu alielewa alikuwa amechoka.

Haikuwa mpaka miaka mingi baadaye nilipo elewa nguvu ya mama muombaji. Ninavyo tafakari juu ya maisha yangu, naona matukio mengi ambapo vitu vingeweza kwenda vibaya sana lakini havikutokea sababu ya maombi ya mama yangu. Kwasababu nilikuwa nime funikwa kwa maombi, ninajua niliepushwa hali nyingi za hatari.

Kutoka kwa binti aliye funikwa kwa maombi nataka kuhamasisha kila mama kukubaliana na Wathesalonike 5:17: "Ombeni bila kukoma." Hata pale inapoonekana kama watoto wako hawajali kuwa wewe unaomba - endelea kuomba tu. Unapojisikia hakuna matumaini - endelea kuomba tu. Kunapokuwa na siku ambazo hauhisi kama Mungu anasikiliza - endelea kuomba tu.

Kama mtu mzima ninathamini kumbukumbu ya mama yangu akisali kwa ajili yangu. Nina shukuru alifanya kama Wakolosai 4:2 inavyosema, "Dumuni katika sala." Nikifikiria mama yangu akapiga magoti kwenye kiti kile kila jioni, machozi ya shukrani hujaa macho yangu.

Akina mama, endeleeni kuomba tu!

Kumbuka: Tiffini Countaway ni Web Producer wa MyHopeRadio.com. Yeye na mume wake Andrew wanaishi St. Louis na wana paka kwa jina la Callie.

Kutoka kwa Mhariri

Debbie Akers

Mungu anatenda maajabu!

Imekuwa lengo langu na maono tangu mara ya kwanza kuulizwa kuanzisha jarida hili kwamba liwe linapatikana katika lugha mbalimbali. Mungu ni anafungua milango mingi na jarida hili sasa linapatikana kwa Kiingereza, Kihispania, Kifaransa, Kijerumani, Kiholanzi, Kireno, Kirusi, Kigiriki, Kiarabu, Kiajemi, Kicheki, Kichina, Kiswahili, Hungarian na Tagalog. Shukrani za pekee kwa Dada zangu Dianna Tuttle na Jerolyn Kelley na timu ya Watafsiri wanaofanya jambo hili liwezekane kila mwezi! Pia, Mchungaji Don Hanscom anashughulikia kutafsiri katika lugha ya Urdu, Hindi, Thai, Tamil, Kisinhali na Kilaotiani! Tunaangalia kuongeza Kipolishi, Kiromania na Kiitaliano.

Hivyo chini ya uongozi wa Dada Gwyn Oakes, Raisi wa UPCI Ladies Ministry, kuwakilisha dhamira yetu ya maombi kwa ajili ya watoto wetu duniani kote bora, kuanzia sasa tutakuwa tukijulikana kama Wamama wa Maombi wa Kimataifa. Tunafuraha na tunazidi kumwomba Mungu aendelee kubariki huduma hii ya maombi. -Debbie Akers, Mratibu na Mhariri wa Wamama wa Maombi wa Kimataifa

Tafadhali tuma shuhuda na mawazo juu ya maombi kwa MothersOfPrayerIntl@aol.com au debiakers@aol.com

Kutoka Lebanon

Salamu kutoka Byblos!

Asante kwa yote utendayo kufanya MOPI ya Kiarabu ukweli. Kiarabu ni muhimu sana na sisi tumekitumia kuanzisha mkutano kila mwezi na tunapata maslahi kutoka kwa watu ambao hawaendi kanisani mara kwa mara au hawajawahi kuhudhuria. Pia tunatumia jarida hili kila mwezi katika Shule ya Biblia. Wanafunzi kisha hushirikiana na wengine.

Kwa sasa tunatumia jarida la Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kireno na Kitagalog. Tuna nakala za ziada kuwapa wageni na kuwashirikisha (wazo la 'kuomba kwa ajili ya familia' daima hupata mwitikio chanya huko Kati-Mashariki.)

Jambo jingine ambalo ni la ajabu kuhusu MOPI - ni nyenzo kubwa kwa maslahi ya wageni. Mwezi uliopita nilizindua makundi ya mwezi ya maombi katika maeneo tofauti ya kijiografia kwa kutumia nyumba za akina mama ili waweze kukaribisha marafiki zao pia ambao si wahudhuria huduma.

Asante tena kwa msaada wako katika kufanya hili kutokea.

Upendo wa dhati wa Kikristo kutoka Lebanon,
Mariann Starin

Amali 31 za Biblia za kuomba kwa ajili ya watoto wako (22-24)

22 Ridhaa - "Baba, wafundishe watoto wangu siri ya kutosheka katika lolote na kila hali, kupitia Yeye ambaye huwapa nguvu kwao." (Wafilipi 4:. 12-13)

23 Imani - "Naomba imani ipate mizizi na kukua katika mioyo ya watoto wangu, kwamba kwa imani waweze kupata kile ambacho kimeahidiwa kwao." (Luka 17: 5-6; Waeb 11: 1-40).

24 Moyo wa Mtumishi - "Mungu, tafadhali wasaidie watoto wangu kuendeleza mioyo ya mtumishi , ili waweze kutumika kwa moyo wote, kama vile wanamtumikia Bwana, na si wanadamu" (Efe.6: 7)

Imewasilishwa na Gwyn Oakes. Hati miliki Bob Hostetler (www.bobhostetler.com). Imetumiwa kwa ruhusa ya mwandishi.

Kwa Mengineyo

Pentecostal Publishing House
Mothers of Prayer Intl
UPCI Ladies Ministries
Reflections
Today's Christian Girl
More to Life Bible Studies
World Network of Prayer
UPCI
My Hope Radio
Multicultural Ministries

Forward this issue



Maisha Safi..... $10

Wasichana wa miaka yote wanahitaji majibu ya uaminifu. Maisha Safi ni kitabu kitakacho wapa zana na msukumo wanaohitaji kufanya maamuzi muhimu ambayo yanaweza kuunda mustakabali wa maisha yao. Utakaso ni suala la moyo. Ni suala la akili. Ni suala la kiroho. Ni suala la kimwili. Wasomaji wa kitabu hiki watajifunza jinsi ya kutumia amri muhimu kuliko zote, kumpenda Bwana Mungu wao kwa moyo wote, nafsi, akili na nguvu zao zote.

Kuweka oda piga simu 314.837.7300 muulizie Jane Buford